




## DEPARTMENT OF ECONOMIC SECURITY

Your Partner For A Stronger Arizona



# ARIZONA DEPARTMENT OF ECONOMIC SECURITY NOTISI YA SHERIA YA WAMAREKANI WENYE ULEMAVU



Ikiwa una ulemavu au matatizo ya kiafya, afya ya akili, au matatizo ya kujifunza ambayo yanayozuia unachoweza kufanya, una haki chini ya Sheria ya Wamarekani wenye Ulemavu (Americans with Disabilities Act, ADA). Sheria ya Wamarekani wenye Ulemavu (ADA) inawalinda watu walio na hali hizi na nyinginezo:

- Hali za kiafya (ugonjwa wa moyo, saratani, pumu, HIV, nyinginenezo)
- Matatizo ya kujifunza
- Mfadhaiko na hali zingine za afya ya akili
- Matatizo ya kusikia, kuzungumza na kuona

Ikiwa una ulemavu au matatizo ya kiafya, afya ya akili, au matatizo ya kujifunza, unaweza kuwa na haki ya huduma maalum kutoka kwa Idara ya Usalama wa Kiuchumi (Department of Economic Security, DES), huduma maalum zinaweza kuwa:

- Msaada katika kujaza fomu
- Msaada katika kuelewa sheria za mpango
- Vifaa na huduma (k.m., wakalimani wa lugha ya alama, wasomaji, n.k.)
- Nyenko za Nukta nundu, maandishi makubwa, kwenye kaseti au CD
- Miadi ya wakati au mahali tofauti, au nyumbani kwako
- Kubadilisha kanuni za mpango
- Kukusaidia kwa njia zingine

Ili kuomba huduma maalum, muulize mfanyakazi wako au Mratibu wa Nje wa ADA katika Idara.

**Unaweza kuwasiliana na Monique Perry, Mratibu wa Nje wa ADA katika Idara, kwa anwani, barua pepe au nambari ya simu iliyopo hapa chini.**

### DES Office of Equal Opportunity

1717 W. Jefferson Street, Ste. 103  
Mail Drop 1119  
Phoenix, AZ 85007  
[oeoada504coordinator@azdes.gov](mailto:oeoada504coordinator@azdes.gov)

**Simu:** (602) 364-3976 – TTY: 7-1-1

**Faksi:** (602) 364-3982

Ukiomba huduma maalum na usiipate au ikiwa unafikiri kuwa Idara ya Usalama wa Kiuchumi (DES) imekuhudumia kwa njia isiyo ya haki kwa sababu ya hali yako ya kiafya au ulemavu, una haki ya kuwasilisha malalamiko kwa Mratibu wa Nje wa ADA katika Idara. Unaweza kuwasilisha malalamiko kwa barua, kwenye fomu ya malalamiko ya DES, au kwa simu.

### Tafadhali Kumbuka:

- Nakala za hati hii zinapatikana katika muundo wa Nukta Nundu, maandishi makubwa, au miundo mingine kulingana na ombi.
- Sheria ya Wamarekani wenye Ulemavu (ADA) haihitaji Idara ya Usalama wa Kiuchumi (DES) kuchukua hatua yoyote ambayo inaweza kubadilisha asili ya mipango au huduma zake, au kuweka mzigo usiofaa wa kifedha au wa usimamizi.

Mwajiri / Mpango wa Fursa Sawa • Misaada na huduma za ziada zinapatikana zinapoombwa kwa na wenyewe ulemavu  
• Huduma za TTY/TDD 7-1-1 • Disponible en espanol en linea o en la oficina local.